

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
10 Januari 2009**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mwishehe  
Bashiri Rashidi  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Idrisa Kessi Zongo  
John Emil Maximilian  
Juma Ali Salehe Jongo  
Juma Hassan Chibaya  
Kibwana Mohammad Msiga  
Mohammed Samwely  
Paulo Atibu Hatibu  
Shamte J Kigoma

**Sherehe kwa walemavu**

Maximilian alisema kuna tukio kubwa kwa walemavu Diamond Jubilee, Upanga jumapili wiki ijayo. Tulikubali kutengeneza vipeperushi na Maximilian atajaribu kutupatia nafasi kwenye ratiba kwa UWABA kuongea.

**Volunteer**

Shirika la kijerumani ambao wanatumia volunteer kwa TASEA walipiga simu kusema kwamba UWABA haifai kama NGO kupokea volunteer kwa sababu hatuna ofisi kubwa wala wafanyakazi wa kila siku.

**Shiriki la kibarua la baisikeli**

Elaine alifanya utafiti kwenye intaneti na alitumia emails kuhusu wazo la shiriki la kibarua la baisikeli. Alipata shirika la dunia la watu wanaofanya biashara hii na aliwasiliana nao na wapo tayari kutupa ushauri. Pia alitembelea wizara ya kilimo na ushiriki kupata taarifa kuhusu kuandaa shiriki lakini alichelewa mchana na maofisa hawakuwepo. Idrisi alisema atatembelea ofisa ya mkoa ya ushiriki Ilala Boma. Tuliongea kuhusu kuruhusu shiriki kutumia ofisi ya UWABA mwanzoni.

**Repoti ya msafara wa baisikeli**

Elaine alimpa nakala ya repoti kwa Mejah iliapeleke Business Times.

**Mradi wa Wamba**

Tutanedelea kufuatalia na mfumo wa Wamba kupata sehemu ya pili ya fedha. Elaine aliongea na mwalimu Emmanuel wa Kigamboni Secondary School na alisema ataongea na mwamlimu mkuu kuhusu siku gani na saa ngapi zitafaa kwa mafunzo.

### **Video ya usalama wa baiskeli**

Elaine alipata rafiki ambaye ana software kutengeneza DVDs na anashughulika kuweka video kwenye DVD. Hamadi alisema ana rafiki anayejua kuhusu videos kutusaidia kutengeneza video zingine – ni nzuri aje kwenye mkutano.

### **Mkutano na serekali ya jiji na kongamano**

Juma aliangalia sanduka la posta na hakuna jibu kutoka serekali ya jiji bado. Filbert atafuatalia wiki hii.

Ubalizi wa Uholonzi walimwambia Elaine wapo tayari kusaidia kuanzisha kongamano kwa kutoa sehemu ya mkutano na chakula cha mchana kwa washiriki.

### **Foundation for Civil Society**

Elaine alitembelea British Council na alipata taarifa kwamba kozi ya kiingereza pale ni Tsh 340,000 kwa mtu pamoja na kupima kabla ya kuanza. Kama tunalenga watu 20 basi hii itazidi Tsh 5,000,000. Tuliongea kuhusu kuanza na kozi ya kompyuta au kozi ya kiingereza na tuliambia kuanza na kozi ya kompyuta. Tulitembelea Argentina internet café na tuliona ni bei nafuu zaidi kulipa kwa saa kuliko kwa mwezi. Ni Tsh 700 kwa saa kwa kompyuta za intaneti na Tsh 500 kwa saa kwa kompyuta bila intaneti. Elaine ataandaa fomu ya kuomba hela na tutapitia pamoja wiki ijayo.

### **Wizara ya Miundombinu**

Idrisi alipeleka barua kwa Wizara ya Miundombinu.

### **NSSF**

Mejah alipeleka nakala nyingine ya barua kwa NSSF na walisema hawakupokea barua ya kwanza. Tutasubiri muda halafu tutafuatalia tena.

### **Service Roads**

Elaine aliandaa barua kwenda kwa TANROADS kuwapongeza kuhusu alama za barabarani kwenye sehemu za hifadhi za barabara, na wanachama walisahihisha barua. Hamadi atapeleka nakala kwa TANROADS Dar es Salaam, Ubungo na Paulo atapeleka kwa TANROADS makau makuu mjini.

### **Wikipedia**

Mtu anayeandia wikipedia ya kiswahili aliandika makala kuhusu UWABA na alimwambia Elaine akaona.

### **Mambo ya hela na guta**

Ally Saidi Mwishehe alisema hataweza kuwa meneja wa guta zaidi kwa sababu biashara siyo nzuri na anaogopa deni. Bado atalipa Tsh 21,000 inayodaiwa. Tulikubali kwamba Filbert akae na guta wiki hii na wiki ijayo mwanachama yeyote atapenda kuwa meneja aje na dereva kuomba nafasi hii

Ada ya mwaka ya sanduka la posta inadaiwa Tsh 30,000. Tulikubali Juma alipe kutoka kwa Tsh 40,800 ya hela ya UWABA anayo.

**Kuwahi mkutano**

Tunaona wanachama wengi hawafiki mkutano mpaka saa tano hata kama saa ya kuanza mkutano ni saa nne. Tulikubali kuwahi.

**Corporal Abuu**

Elaine aliuliza traffic police kuhusu Corporal Abuu amelazwa hospitali gani na yupo Muhimbili Moi. Juma alimtembelea na alimpa kila ya kheri kutoka UWABA.

**Baiskeli kutoka UK**

Kuna mashirika UK ambao wapo tayari kututumia baiskeli lakini lazima sisi tulipe meli na kodi. Wanachama watatafuta taarifa kuhusu gharama hizi.

**Mambo mengine**

Elaine ataandaa kitambulisho kwa Maximilian na ataleta kamera kutengeneza vitambulisho kwa wengine wanaohitaji.

Elaine alimpigia simu Rashid ambaye yupo kwenye mkutano lakini hajaja mkutano muda mrefu. Alisema atakuja wiki ijayo.

Tutamsubiri Mejah aje mkutano kuomba ushauri kuhusu mashindano ya wimbo.

Jumanne anaumwa muda mrefu na amerudi Tanga.